



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA



Barua zote ziadikwe kwa:  
Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya  
Simu nambari:+255 (026)- 2702585/2702828  
Nukushi, +255(026)-2701776/2700580/270175

S.L.P. 108,  
IRINGA.  
TANZANIA

Baruapepe:ded@iringadc.go.tz  
Tovuti: www.iringadc.go.tz

Kumb.Na. IDC/S.20.45/26

04.09.2024

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI 40**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa anapenda kuwatangazia wananchi wote wenye sifa na nia ya kufanya kazi ya Ajira ya Muda (Vibarua) kwa nafasi ya;-

**1.0 Wakusanya Mapato**

**2.0 SIFA ZA MWOMBAJI**

- i. Awe raia wa Tanzania mwenye umri zaidi ya miaka 25.
- ii. Awe amemaliza kidato cha nne.
- iii. Awe na uwezo wa kutumia simu janja (Smart Phone).
- iv. Awe muadilifu na hajawahi kushtakiwa kwa kosa lolote
- v. Awe tayari kufanya kazi maeneo ya Vijijini
- vi. Awe na barua za wadhamini watatu wenye mali zisizohamishika, majina saini za Mtendaji wa Kijiji/Mtaa na Mwenyekiti wa Mtaa/Kijiji ikiambatana na picha moja ya mdhamini, namba ya nida, cheti cha kuzaliwa na nakala ya cheti cha Kidato cha Nne, mwombaji aambatishe picha mbili zilizopigwa muhuri na mtendaji wa Kijiji/Mtaa.
- vii. Mwombaji atakayewasilisha taarifa na sifa za kugushi atachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

**KAZI/MAJUKUMU**

- i. Kukusanya ushuru unaotokana na mapato na tozo mbalimbali za Halmashauri
- ii. Kuhakikisha fedha zote zilizokusanya kwa siku hiyo zinapelekewa benki
- iii. Kuhakikisha mapato yote yanakusanya kwa kutumia mashine ya POS na kutoa risiti halali ya Halmashauri ya Wilaya ya Iringa
- iv. Kufanya uhakiki na ukaguzi wa mizigo na malipo ya ushuru natozo katika maeneo ya kazi
- v. Kuchukua hatua stahiki kwa yejote atakaekiuka sheria na taratibu
- vi. Kufanya shughuli nyingine utakazopangiwa namsimamizi wako

**MALIPO/MSHAHARA**

Malipo ya mshahara yatakuwa Tshs. 10,000/= kwa siku na malipo yatafanyika mwisho wa mwezi ambayo ni Tshs. 300,000/= kwa mwezi, Aidha Mkataba huu utadumu kwa muda wa miezi mitatu tu.

Maombi yatumwe kwa;

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa,

S. L. P 108,

**IRINGA.**

Mwisho wa kutuma maombi ni **tarehe 19.09.2024** saa **09:30** alasiri

Tangazo hili limetolewa na;

Robert M. Masunya  
**MKURUGENZI MTENDAJI (W),**  
**IRINGA.**  
**MKURUGENZI MTENDAJI**  
**HALMASHAURI YA WILAYA**  
**IRINGA**